**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOBA**
***Shule ya Sekondari Nyakato, S.L.P 06, Bukoba***

Namba za simu:
Mkuu wa shule: 0622494456/0784464021
Makamu mkuu wa shule: 0625912520/0753934227
Patron: 0755205608
Barua pepe: secondarynyakato@gmail.com

Tarehe …………….

Mzazi/Mlezi wa…………………………………………
S. L. P …………………………………………………..

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NYAKATO HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOBA MKOA WA KAGERA MWAKA …………….**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka ………………….. Katika shule hii kuna tahasusi za **HGK, HKL, PGM, CBG, PCM, HGE na PCB.**

Shule ya sekondari Nyakato ipo umbali wa kilomita 6 kusini mwa mji wa Bukoba. Nauli ya kutoka mjini hadi kufika shuleni si zaidi ya **Tsh. 4000/-** kwa pikipiki au **Tsh. 7000/-** kwa bajaji.

Muhula wa masomo utaanza tarehe ……………**,** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ……………….**.** Mwisho wa kuripoti ni tarehe ………………**.**

**2 Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Kila mwanafunzi aripoti shuleni akiwa na bima ya afya/au Tsh. 50,400/-.**

**2.2 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni suruali mbili nyeusi zinazofunika soksi zenye upana usiopungua **sentimeta 18** chini.
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi.

iii. Sare ya michezo ni "**track suit" ya kijani** yenye michirizi myeupe isiyo na maandishi yoyote, bukta 3 ya rangi ya **bluu** yenye michirizi myeupe na raba za michezo.
iv. Viatu vyeusi jozi mbili vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeusi za shule.
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali.
vii. Sweta moja ya rangi ya **maroon**.
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) ni suruali moja ya rangi ya **kahawia** (ugoro) inayofunika soksi na upana usioungua sentimita 18 chini.
ix. **t-shirt mbili (2)** za rangi ya njano zenye kola na zisizo na maandishi zinauzwa kwenye maduka ya mavazi, endapo hatazipata zinapatikana kwenye maduka karibu na shule kwa bei ya Tsh.15,000 kila moja.
x. Mwanafunzi afike shuleni akiwa amevaa yunifomu kamili, shati jeupe, suruali nyeusi na viatu vyeusi **nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa shuleni.**

**2.3 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 15 (counter books 8 quire three kwa ajili ya masomo darasani na counter books 7 za quire two kwa ajili ya mazoezi ya kila siku).
ii. **Ream (A4)** ya karatasi mbili (2) kwa mwaka.
iii. Graph pad 1 ya karatasi yenye kurasa 50 (kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi na Jiografia) na box file 1 kubwa kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zake za masomo.
iv. Mkebe wa hisabati (mathematical set) kwa tahasusi za sayansi na Jiografia.
v. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa*).
vi. dissecting kit kwa wanafunzi wanaosoma biology.
vii. Scientific calculator function fx=991 zinapatikana kwenye maduka ya yanayouza vifaa vya shule, endapo atakosa zinapatikana kwenye maduka yaliyopo karibu na shule kwa bei ya Tsh.45,000 kila moja.
viii. Godoro moja futi mbili na nusu kwa inchi tatu, mashuka jozi 2 rangi ya pinki, blanketi 1 na chandarua na taa ya sola.
ix. Mafuta ya kujipaka, taulo, malapa, sabuni za kutosha, mswaki na dawa ya meno.
x. Sanduku moja imara lililotengenezwa kwa bati na "toilet papers" za kutosha.
xi. Sabuni ya maji lita 2 na brush kwa ajili ya usafi wa vyoo.

xii. Mwavuli 1 na viatu vya mvua (rain boots).
xiii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kikombe na kijiko).
xiv. Ndoo 2 ndogo (lita kumi) zenye mifuniko.
xv. Kwanja 1, jembe na mpini wake, kwa tahasusi zote.
xvi. Reki 1, panga 1 na kotama kwa tahasusi za **PCM**, **PGM na HGE**.
xvii. Seti ya ndoo ya kudekia kwa tahasusi za **HGK, PCB, CBG na HKL**.
xviii. Squizer 1, softbroom 1, hardbroom 1 na chelewa, kwa tahasusi zote.

### 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Malipo haya yafanyike kwenye akaunti ya shule namba **31801100049** yenye jina **Nyakato Secondari school recurrent account** ya Benki ya **NMB** na mwanafunzi afike shuleni na risiti ya malipo.

## 3.Sheria na kanuni muhimu za shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na

### 3.1 Sheria na kanuni za shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( morning and evening preparations).
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
ix. Kutunza mali za shule.
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari au muuguzi wa shule
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa mkuu wa shule. (msiba au ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na:**

i. Wizi.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Kufuga ndevu.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.
viii. Uvutaji wa sigara.
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa.
x. Kusababisha mimba.
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi kinyume cha taratibu, sheria na kanuni za shule.

xiv. Kudharau bendera ya taifa.
xv. Kudharau wimbo wa taifa.
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu.
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4.Viambatisho na fomu muhimu**

i. Fomu ya uchunguzi wa afya (medical examination form) ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali;
ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.
iv. Wakati wa kuripoti mwanafunzi awasilishe nakala**(photocopies)** za matokeo ya kidato cha nne **(result slip)** na cheti cha kuzaliwa**(birth certificate)**
**v.** Bandika picha za wazazi/walezi kama inavyoelekezwa kwenye **KIAMBATISHO B** ukurasa wa 8, aidha picha(passport size) ya mwanafunzi ibandikwe upande wa juu kulia kwenye fomu hiyo(**KIAMBATISHO B) ukurasa wa 8.**

**NB: Hakikisha viambatanisho vyote vinavyotakiwa kujazwa vimejazwa kwa usahihi na kukabidhiwa shuleni wakati wa kuripoti**.

**5.** Tafadhali, soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**......................**
**ROBERT M. KASAAJU**
**MKUU WA SHULE**

**ANGALIZO: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- ➢ **Mkuu wa Shule: 0622 494 456**
- ➢ **Makamu Mkuu wa Shule: 0625 912 520/0779223142**
- ➢ **Mwandamizi Taaluma: 0753 483 461/0620 852 844**
- ➢ **Mwandamizi Malezi: 0654 877 883**

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi ……………………………………..mzazi/mlezi wa …………………………...nimezisoma sharia za shule nikiwa na mwanangu na kujadili pamoja naye na amezielewa. Ninakubaliana kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi ya mwanangu na nitakubaliana na adhabu yoyote itakayoamuliwa na uongozi wa shule pale mwanangu atakapokiuka mojawapo ya sheria na kanuni hizi.

Saini ya mzazi/mlezi…………………………………tarehe…………………………………

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi ……………………………..wa kidato cha ……….. nimesoma kwa makini sheria na taratibu za shule nikiwa na mzazi/mlezi wangu. Nimejadiliana naye na nimeelezwa vizuri kabisa, ninaahidi kuwa nitazifuata na endapo nitakiuka mojawapo ya sheria na taratibu hizi hatua zichukuliwe dhidi yangu. Ewe mwenyezi Mungu nisaidie.

Saini ya mwanafunzi……………………………Tarehe ……………………………

Ni imani yangu kuwa utafuata hizi sheria ili uweze kujifunza kwa bidii na kwa mafanikio yaliyo bora. Nakutakia kila la heri na karibu sana Nyakato Sekondari.

…………………
ROBERT M. KASAAJU
**MKUU WA SHULE**

***KIAMBATISHO B***

*Shule ya Sekondari Nyakato*

*S. L. P 6, Bukoba. Simu: 0622494456/0784464021*

Barua pepe: **secondarynyakato@gmail.com**

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Jina la mwanafunzi…………………………………………………………………………………….
2. Tarehe ya kuzaliwa ………………………mwezi……………………..mwaka…………………….
3. Mahali alipozaliwa: mkoa ……………………… wilaya…………………………………………….
   tarafa……………………………kata …………………kijiji/mtaa………..................................
4. dini………………………………… dhehebu………………………………………………………..

5. Jina la baba mzazi/mlezi………………………………………………wa S.L.P…………………..
   mkoa……………wilaya……………kata……….. namba yake ya simu…..……………………..
   kazi ya baba mzazi/mlezi……………………………………………….
   Yuko hai? Ndiyo/ hapana (kata isiyohusika)

6. Jina la mama mzazi/mlezi………………………………………kazi yake………………………….
   namba yake ya simu……………………………….sehemu anayoishi, mkoa…………………
   wilaya……………………tarafa……………..kata……………………kijiji/mtaa………………...
   Yuko hai? Ndiyo/hapana (kata isiyohusika)

| *Bandika picha ya baba mzazi/mlezi* | *Bandika picha ya mama mzazi/mlezi* |
|---|---|

7. Ndugu wa karibu aliyeridhiwa na mzazi/mlezi anayeweza kupewa taarifa/matatizo ya mwanafunzi kwa haraka endapo mzazi/mlezi hatapatikana.
   Jina kamili…………………………………anuani………………………..
   namba yake ya simu……………………………………
   kazi yake …………………uhusiano na mwanafunzi………………mahali anapoishi…………..

| ***Bandika picha ya ndugu wa karibu*** |
|---|

***KIAMBATISHO C***
**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**NAMEO F STUDENT…………………………………………………………………………**

To medical officer **I/C** of
………………………………………..District/ Regional/Referral/Designated Hospital,
**P.O BOX**…………………………..

**Please examine the above named in full as to his physical and mental fitness for being able to pursue two years of secondary school education. In case of an acute defect/disability in each category or subcategory may render the applicant ineligible of admission or eligible of admission to schools of students with special needs:-**

i. Blood pressure………………………………………………………………….

ii. Sickle cell test…………………………………………………………………...

iii. (a) Eyesight…………………………………………………………………..

(b) Spleen…………………………………………………………………………...

(c) Hearing…………………………………………………………………………

(d) Veneral diseases…………………………………………………………………..

(e) Lepsory…………………………………………………………………………

(f) Typhoid…………………………………………………………………………

iv. Neuroses…………………………………………………………………………….

v. Other serious disease……………………………………………………………

General comment(s)…………………………………………………………………..

Name………………………………………………………………………….
Designation…………………………………………………………………………
Official stamp…………………………… date……………………………………

**ANGALIZO**: mzazi athibitishe kuwa vipimo hivi vimefanyika kikamilifu na siyo kujaza jina na saini ya mganga. Atakayegundulika kuwa hakuchukua vipimo kihalali atarudishwa nyumabani.

***KIAMBATISHO D***

*Shule ya Sekondari Nyakato*
*S. L. P 6, Bukoba. Simu: 0622494456/0784464021*
Barua pepe: **secondarynyakato@gmail.com**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI**

Mimi……………………………………………nakubali nafasi ya kidato cha tano niliyopewa na shule ya sekondari Nyakato. Ninaahidi kutii na kufuata kwa uaminifu sharia, kanuni na taratibu zote za shule, kujifunza kwa bidii, juhudi na maarifa kwa uwezo wangu wote ili kutimiza lengo la kufaulu kwa kiwango cha juu kwa faida yangu, familia yangu na Taifa kwa ujumla. **Ninaahidi kuripoti shuleni nikiwa nimevaa yunifomu kamili kama ilivyoelekezwa na kwa siku iliyopangwa bila kuchelewa**.

Saini ya mwanafunzi……………………

Tarehe ……………………………………

## ORODHA YA VITABU VYA KIADA VINAVYOPENDEKEZWA

Ili mwanafunzi aweze kupata elimu bora na yenye kumwezesha kukabiliana na mazingira halisi ya maisha anapaswa kuwa na vitabu. Ifuatayo ni orodha pendekezwa.

1. KISWAHILI
   - Vuta N'kuvute - Shafi Adam Shafi
   - Mfadhili - Hussein Tuwa
   - Usiku Utakapokwisha - Mbunda Msokile
   - Kufikirika - Shaaban Robert
   - Kwenye Ukingo wa Thim - Ebrahim Hussein
   - Morani - Emmanuel Mbogo
   - Kivuli Kinaishi - Said Mohamed
   - Nguzo mama - Penina Mhando
   - Kimbunga - Haji Gora Haji
   - Mapenzi Bora - Shaaban Robert
   - Fungate ya Uhuru - Mohamed S. Khatibu

2. **CHEMISTRY**
   - Chemistry part 1, Test book for class XI (S.Chands)
   - Chemistry part 2, Test book for class XII (S.Chands)
   - Advanced Chemistry 1 review (problems and solutions)
   - Advanced Chemistry 2 review (problems and solutions)
   - Chemistry for A' level (fouth edition) by RAMSDEN
   - Conceptual Chemistry class XI by S. Chand
   - Conceptual Chemistry class XII by S. Chand

3. **BIOLOGY**
   - Advanced Biology for Secondary Schools – ( Michael R.)
   - Verma P.S and Pandey P.B (2010) S. Chands for class XI
   - Cell structure and organization - L. Msaki
   - Taylor el al (2006(Biological science, third edition, Cambridge University Press.
   - Glenn and Toole S.(1999), Understanding Biology for Advanced level, fouth edition, Stanlet Thornes Publishers Limited
   - Verma P.S and Pandey P.B (2006) S. Chands for class XI, first edition, India, S. Chands and Company Limited.

4. **ADVANCED MATHEMATICS**
    - Pure Mathematics 1& 2 - Backhouse
    - Advanced Level Mathematics: By C.J. Tranter
    - Mathematics for A level (volume 1&2) S. Chands
    - Advanced level Mathematics vol.1) – L.K Shayo

5. **HISTORY**
    - Mastering advanced level history book I &11 – Kato 2010
    - Basic themes in European Advanced Level History I&II – Ismail Ngobi - 2012
    - Major events in African History paper I – Fr.Jovitus F. Kamala
    - Towards Rural Development of Tanzania – by C.K Omary
    - Ujamaa – Essay on socialism – By J.K Nyerere
    - How Europe underdeveloped Africa - By Wolter Rodney
    - A histry of East Africa – By E.S Atieno Odhiambo, T.I Ouso & J.F.M Williams
    - A history of Africa (volume I) by Assa Okoth
    - A history of Africa (volume II) by Assa Okoth
    - Basic themes in Advanced level History, paper 1&2 – by F.M Mavunde
    - Advanced level History, paper 1&2 – by Zisti Kamili
    - Contemporary Historical Events, Paper 1&2 by Mwl.Shibitali C.K Tumaini.

6. **ENGLISH LANGUAGE**
    - Oxford Advanced Learner's Dictationary (12th edition)

7. **GEOGRAPHY**
    - General geography in diagrams – R.E Bunnet
    - Practical geography for Africa – John M.Pritchard
    - Physical geography for Africa – D.T Msabila
    - Human and Economic geography - D.T Msabila

8. **PHYSICS**
    - S.Chands Principals of Physics for class XI & XII
    - Principal of physics - Rogers Municaster
    - Advanced Level Physics – Nelkon & parlker
    - Principles of physics – Tom Duncan
    - A – level physics – Roge Municaster (4th Edition)
    - Comprehensive Physics (volume I & II)